**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI.**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI.**

SHULE YA SEKONDARI
MIYOMBWENI,
S. L. P 145,
MBARALI – MBEYA
TAREHE ....................

KUMB. Na. ..........................................................

JINA LA MWANAFUNZI ..............................................
S. L. P ..................................................................
............................................................................

**YAH:- MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIYOMBWENI WILAYA YA MBARALI MKOA WA MBEYA MWAKA ...............................**

1. Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka ............................... shule ya sekondari Miyombweni ipo umbali wa mita 200 Magharibi mwa barabara kuu toka Rujewa kwenda Madibira wilaya ya Mbarali.
2. Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ...................................... unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ............................... (ndani ya siku saba ukichelewa zaidi hutapokelewa)
3. Bidii ya kujituma katika masomo, utii, uaminifu, nidhamu bora, maarifa na ujuzi kwa pamoja/ujumla vitakuwezesha kuwa na mafanikio mazuri kitaaluma na kujijengea tabia na mwenendo mzuri endelevu.

## 1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
## SARE YA SHULE

### 1.1. WAVULANA.

i. Suruali mbili (2) moja rangi ya kaki na nyingine rangi ya damu ya mzee. Suruali ziwe zina malinda mawili (2) mbele. Tafadhali.
ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
iv. Soksi rangi nyeusi zisizo na pambo au mapambo yoyote yale.
v. Mkanda wa kiunoni wa kuvalia suruali uwe wa ngozi rangi nyeusi
vi. Sweta (2) rangi ya Kijani na damu ya mzee tafadhali liwe jipya.
vii. Bukta rangi ya Bluu na tisheti ya rangi ya bluu kwa ajili ya michezo
viii. Viatu vya michezo.

## 2.0. WASICHANA.

i. Sketi mbili moja ya rangi ya kaki na nyingine rangi ya damu ya mzee. Tafadhali sketi zote mshomo wake ziwe za malinda na ziwe ndefu sana.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi
iv. Soksi rangi nyeupe zisizo na pambo au mapambo yoyote yale
v. Sweta ya rangi ya kijani na damu ya mzee. Tafadhali liwe jipya
vi. Hijabu rangi nyeupe.
vii. Bukta ya rangi ya Bluu na tisheti ya rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.
viii. Viatu vya michezo

***NB: "Mwanafunzi ambaye sare yake haitakidhi matakwa ya shule hatavumiliwa"***

2.1. Daftari kubwa 9 kaunta Quire 2 au Quire 3 na mkebe 1 kwa kila mwanafunzi, daftari ndogo 9
2.2. Chakula cha mchana, matibabu endapo mwanao ataugua akiwa shuleni ni juu ya mzazi.

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MHIMU ZA SHULENI.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini vipindi vyote vya darasani.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za umma.
i) Mwanafunzi asimame wakati mwalimu au mtu yeyote anayemzidi anapopita au kuingia darasani.
j) Usizungumze na mwalimua au mtu yeyote anayekuzidi umri ukiwa umekaa, mikono mifukoni ama kofia kichwani ama ukiwa umevaa miwani ya jua.
k) Mwanafunzi huruhusiwi kutembea usiku bila sababu wala kuingia video
l) Mwanafunzi huruhusiwi kuvaa nywele za bandia wala kutumia rangi za kucha na midomo.
m) Haifai kwa mwanafunzi kuvaa nguo zinazoonesha mwili wala nguo fupi
n) Usichelewe siku za kufungua shule au usiongeze siku za ruhusa
o) Usigune wakati mwalimu au kiongozi anatoa tangazo.

**3.2.Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli,viloba n.K
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa/kuolewa.
j) Kutoa mimba
k) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

**Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

a) Fomu ya Medical Examination ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hizi zitakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi utakaporipoti shuleni

FLAVIAN E. DAFTARI
MKUU WA SHULE
0764 948443
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MIYOMBWENI
S.L.P. 145, RUJEWA

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**

MIYOMBWENI SECONDARY
SCHOOL,
P. O. BOX 145,
RUJEWA – MBEYA.
DATE ..................................

REF. NO. MSS/JI/1/02 ..................................
THE MEDICAL OFFICER
..........................................................
..........................................................
..........................................................

Please examine .......................................................................... as for her/his fitness for pursuing further education in this school.

1. Hemoglobin ..........................................................................................
2. P.V Bleeding ........................................................................................
3. (a) Weight ............................................................................................
4. Blood pressure ....................................................................................
5. Urine for sugar and pregnancy ..........................................................
6. Stool ........................................................................................................
7. Asthma ...................................................................................................
8. Skin Disease ..........................................................................................
9. Lepresy ..................................................................................................
10. Eplopsy .................................................................................................
11. Pulmonary ............................................................................................
12. Mental problems ..................................................................................

Comments of the medical officer

.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................
.........................................................................................................................